

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKUU WA MKOA WA NJOMBE

SIMU: 026- 2790001

FAX: 026- 2790001



OFISI YA MKUU WA WILAYA,

S.L.P 02,

LUDEWA.

JUNI 16, 2022

TAARIFA KWA UMMA

Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mheshimiwa Waziri Waziri Kindamba leo Juni 16, 2022 ameshiriki Mkutano wa Baraza la Waheshimiwa madiwani ulio fanyika katika ukumbe wa Halmashauri Ludewa mjini.

Wakati akihutubia Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa ameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kwa mambo mbalimbali ikiwemo ukusanyaji wa mapato lakini pia akaongeza kwa kuwapongeza viongozi wote wa Wilaya ya Ludewa kwa kufanikisha zoezi zima la Anwani za Makazi na Postikodi.

Aidha Mhe. Waziri Kindamba pamoja na kushiriki Mkutano huo amekagua miradi mbalimbali inayotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ikiwemo mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madasa na matundu sita ya vyoo pamoja na nyumba moja pacha ya walimu unaotekelezwa na TASAF uliopo katika kijiji cha Kiyombo.

Sambamba na hayo Mkuu wa Mkoa amesema kuwa leo Juni 16, 2022 ni siku ya Watoto wa Afrika na kwa Wilaya ya Ludewa imefanyika katika Kata ya Ruhuhu hivyo kwa kaulimbiu isemayo Tuimalishe Ulinzi wa Mtoto, Tokomeza Ukatili dhidi yake, Jiandae kuhesabiwa, hivyo amewasihi wananchi wote wa Mkoa wa Njombe kuwalinda watoto na kuhakikisha wanatoa taarifa za ukatili katika vyombo vinavyohusika.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Ludewa amemshukuru Mkuu wa Mkoa wa Njombe kwa kufika katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa na akatumia nafasi hiyo kumkaribisha tena wakati wote.

Chrispin B. Kalinga
Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini
Halmashauri (W) Ludewa